

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI
ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA

Unapojibu Tafadhali taja:

Kumb. Na. MODC/A.10/05/VOL III/49

30 August, 2021.

TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba anawatangazia wananchi wote wenye sifa zilizoainishwa kwenye tangazo hili kuomba nafasi za kazi ya mkataba wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

WAKUSANYAJI WA MAPATO (NAFASI 25)

MAJUKUMU YA KAZI

1. Kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kutumia mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato (**POS**)
2. Kuhakikisha Fedha inayokusanywa inapelekwa Benki kwa wakati (ndani ya masaa 24)
3. Kuhakikisha Mapato yote yanapaswa kukusanywa na Halmashauri yanakushanywa kwa usahihi.

SIFA ZA MWOMBAJI

Mwajiriwa awe na elimu ya darasa la saba na kuendelea, anayejua kusoma na kuandika vizuri awe na uelewa wa kutumia simu ya tachi (**smart phone**), sababu mapato yote ya Serikali yanakusanywa kwa kutumia mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato (**POS**) ambayo inafanya kazi kama simu za tachi.

MASHARTI YA WAOMBAJI KATIKA KAZI HII


1. Awe ni raia wa Tanzania mwenye umri kuanzi miaka 21
2. Waombaji waambatishe cheti cha kuzaliwa
3. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitoshela (detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika
4. Maombi yaambatane na nakala ya vyeti kama umeanisha elimu zaidi ya darasa la saba.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Momba, S. L. P 273, Simu 025-295-747-6, Nukushi 0
Barua pepe ded@mombadc.go.tz, Tovuti www.mombadc.go.tz

5. Maombi yaambatanishwe na majina mawili (2) ya wadhamini wenye mali isiyohamishika na kuanisha mali yenyewe mfano nyumba au ardhi, anwani kamili na namba zao za simu.
6. Awe tayari kupangiwa kituo chochote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Momba.
7. Awe mwaminifu katika kukusanya mapato ya Serikali na kuhakikisha Fedha ya Serikali haipotei.
8. Awe tayari kutii na kufuata maelekezo atakayopangiwa bila kuvunja misingi ya Sheria ndogo za Halmashauri.
9. Mwisho wa kuwasilisha maombi haya ni tarehe 13/09/2021.


Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta, kupitia anuani ifuatayo na nakala itume kwa barua pepe au kuyawasilisha kwenye ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba.

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Momba,
S.L.P 273,
TUNDUMA-MOMBA
E-mail: mombadc.go.tz



REGINA L. BIEDA

MKURUGENZU MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA



NB: Tangazo hili linapatikana kwenye mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Momba na kwenye Tovuti (**website**) ya Halmashauri ya Wilaya ya Momba ambayo ni www.mombadc.go.tz